# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 22302
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA MAWASILINO, ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.

***Mheshimiwa Spika,*** Naomba uniruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma, kwa kutujaalia uzima na kutuwezesha kukutana tena katika Mkutano huu wa Sita, Mkutano ambao ni wa kwanza kujadili Ripoti za Kamati za Kudumu kwa Baraza hili la Kumi la Wawakilishi Zanzibar. Kadhalika nachukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi jinsi unavyokiongoza na kukiendesha chombo hiki pamoja na wasaidizi wako, tunamuomba Mwenyezimungu akujalieni hekima na Busara katika kutekeleza majukumu yenu.

***Mheshimiwa Spika***, Kadhalika nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa kuendelea kuniamini na kunipa imani ya kuwaongoza. na kutoa mashirikiano makubwa, jambo ambalo limenipa nguvu na pia limesaidia kufanikisha vizuri majukumu ya Kamati yetu. Kwa hakika weledi na umahiri wao umesaidia kwa kiasi kikubwa sana kupatikana hadi kuwasilishwa kwa ripoti hii.

**Mheshimiwa Spika,** nakuhakikishia kwamba Wajumbe wangu wamefanya kazi nzuri katika kuhakikisha Kamati inaisimamia vyema Serikali kwa mujibu wa Katiba yetu na maslahi ya Taifa zima. Na hapa napenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe Yahya Rashid Abdullah | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe Hudhaima Mbaraka Tahir | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| 4. | Mhe Fatma Mohammed Ramadhan | Mjumbe |
| 5. | Mhe Kombo Mwinyi Shehe | Mjumbe |
| 6. | Mhe Rukia Omar Ramadhan | Mjumbe |
| 7. | Mhe Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Rahma Kombo Mgeni | Katibu |
| 9. | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Mawasiliano Ardhi na Nishati, ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 107 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020 na majukumu yake ni kama yale yaliyokwisha kuelezwa katika jadweli la kwanza Kamati hii inafanyakazi na Wizara tatu zifuatazo: -

(1) Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi

(2) Wizara Ardhi na Maendeleo ya Makaazi

(3) Wizara ya Maji, Nishati na Madini

## 1) WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati, inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa jitihada zake za kuhakikisha miundombinu ya Usafirishaji pamoja na huduma za usafiri zinaimarika siku hadi siku, hapa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada zinazofanywa na Wizara Kamati inapenda kutoa maoni na Maagizo kupitia Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii kama ifuatavyo: -

***Sekta ya Usafirishaji***

***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Usafiri wa nchi kavu na majini inasimamiwa na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Wakala wa Serikali wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar Pamoja na Mamlaka ya Usafiri Baharini.

a) **Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani.**

**Mheshimiwa Spika,** bajeti ndogo, tatizo la usafiri pamoja na ufinyu wa Ofisi ni miongoni mwa vikwazo vinavyopunguza kasi ya utendaji wa Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani. Aidha deni la Mamlaka kwa Wakala wa Uchapaji.

***Mheshimiwa Spika**,* Ripoti yetu imebainisha na kuchambua kwa kina changamoto za Mamlaka hii na nawaomba waheshimiwa wajumbe wazipitie ili kupata maoni yao. Kamati inashauri kufanyiwa kazi kwa changamoto hizo ikiwemo tatizo la ufinyu wa jengo katika Ofisi ya Pemba.

***Mheshimiwa Spika,*** Vile vile Kutokana na deni kubwa wanalodaiwa Mamlaka kamati inashauri Wizara kufanya jitihada za makusudi kulipa deni hilo ili waweze kupatiwa nyaraka zinazohitajika katika kutekeleza kazi zao kutoka Wakala wa Uchapaji.

**b) Mamlaka ya Usafiri wa Baharini**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati yetu imeridhika na utendaji wa Mamlaka ya Usafiri wa Baharini ambayo ina dhamana ya kusimamia usafiri wa baharini. Pamoja na kuridhika na utendaji wa Mamlaka hiyo, Kamati imebaini tatizo la Ukosefu wa kikosi kazi cha uokozi (***Search and Rescue Organization***) ambacho ni muhimu kuwepo bandarini huku maslahi madogo yanachangia kuwavunja moyo wataalamu wachache waliopo katika Mamlaka hiyo.

***Mheshimiwa Spika,*** katika kuzipatia suluhisho changamoto zinazoikabili Mamlaka hiyo Kamati inaishauri Wizara kuongeza nguvu kazi kwa kuajiri wafanyakazi wenye ujezi na kuwapatia vifaa husika na kuwalipa wanavyostahili. Aidha Kamati inashauri kuchukuliwa hatua suala la uwepo wa kikosi kazi cha uokozi kutokana na umuhimu wake.

***Mheshimiwa Spika,*** pia Kamati inaishauri Wizara kupitia Mamlaka kuangalia uwezekano na kuomba kurudishiwa ruzuku kutoka Serikalini ili Mamlaka iweze kujiendesha na kutatua baadhi ya changamoto ambazo kwa sasa wanashindwa kutokana na uhaba wa fedha.

c) **Wakala wa Serikali wa Karakana Kuu ya Magari**

***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Serikali wa Karakana Kuu ya Magari nayo ni taasisi muhimu katika sekta ya usimamizi wa Usafirishaji, taasisi ambayo imepewa jukumu la kuzifanyia matengenezo Gari za Serikali na Binafsi.

Kamati imeshuhudia mazingira ya kazi yasiyorafiki kiafya na kiutendaji ndani ya Mamlaka hiyo suala ambalo huenda likawa linachangia kuwakimbiza wateja. Kamati pia imeshangazwa na tatizo la ukosefu wa wataalamu mahiri wa gari za kisasa, suala ambalo limepelekea Wakala kuazima fundi kutoka JKU kutokana na kusitishwa uajiri Serikalini.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha na kuchukuliwa jitihada za makusudi kwa bajeti ijayo kuweza kupatikana wataalamu wa magari ili waweze kusaidia na kufanikisha kazi za Karakana Kuu ya Serikali ili kufikiwa lengo la kuundwa kwake.

***Mheshimiwa Spika,*** Katika suala la mapato wanayokusanya Karakana kamati inaishauri Wizara kufatilia na kuweza kupatiwa asilimia ambayo wataweza kuitumia katika kuendeshea kazi zao za kila siku ikiwemo ununuzi wa vifaa vya magari vinavyohitajika.

Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuiangalia Karakana Kuu ya Serikali katika bajeti ijayo kwa kuwatengea fedha za ununuzi wa vifaa ili iweze kujiendesha na kufanikisha kazi zake kama ilivyokusudiwa.

***Mheshimiwa Spika,*** kamati pia inatoa wito kwa Taasisi zote za Serikali kuitumia Karakana Kuu ya Magari kwa kuduma zote za matengenezo ya vyombo vya moto.

**d) Wakala wa Barabara.**

***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti yetu pia imechambua kwa kina Wakala wa Barabara wenye jukumu la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu ya usafirishaji iliyosalama na endelevu. Wakati wa kazi za Kamati tulitembelea barabara mbali mbali Unguja na Pemba na Mtambo wa Lami uliopo Vitongoji Pemba na Kibele Unguja. Katika ziara hizo za Kamati tumebaini changamoto kadhaa ambazo tumeziweka wazi katika ripoti yetu ikiwemo ufinyu wa bajeti katika kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara, Uelewa mdogo wa wananchi katika kulinda hifadhi ya barabara pamoja na Ukosefu wa vifaa vya kazi kwa wajenzi wa barabara ikiwemo nguo na vifaa vya kujikinga. Aidha Kamati inawasiwasi na kasi ndogo ya Mpango wa muda mrefu wa daraja la Uzi Ng'ambwa.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati pia hairidhishwi na sura mbaya inayoonekana katika Barabara zetu nyingi hasa za Mjini kutokana na kujaa mashimo hali amabayo inaleta usumbufu kwa watumiaji na taaswira mbaya kwa nchi.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaishauri Wizara kupitia Wakala wa Barabara kutumia wataalamu wenye ujuzi pamoja na kuwa na mipango ya muda mrefu wakati wa ujenzi wa barabara ili tuwe na barabara zenye ubora na viwango ambazo zinazokidhi haja kimatumizi kwa muda mrefu na kuacha kufanya kazi kwa mazoea. Kamati pia inasisitiza kuangaliwa suala la kupatiwa vifaa vya kufanyia kazi wajenzi wa barabara ikiwemo nguo na vifaa maalum vya kujikinga wakati wakiwa kazini ili kuwa salama kiafya na kuepuka athari ikiwemo kuungua na lami imoto.

***Usafiri wa Bahari na Anga.***

***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Bandari, Shirika la Meli na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ni taasisi zenye jukumu la kuhakikisha kuwepo kwa huduma bora za usafirishaji wa abiria na mizigo katika sekta ya usafiri wa Bahari na Anga. Kamati imebainisha changamoto na kushauri njia bora za kuzitatua kwa kila moja. Nawaomba sana waheshimiwa wajumbe mzipitie kama zinavyoonekana katika Ripoti yetu.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inapongeza ujenzi wa bandari ya Mkokotoni uliokamilika kwa asilimia 95 lakini pia inashauri kukamilishwa kwa maeneo mengine yaliyobakia ikiwemo sehemu ya kupitia abiria, kuwekwa uzio, barabara na sehemu za kuhifadhia mizigo ili iweze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa na kuiingizia fedha Serikali zitokanazo na makusanyo na tozo.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inatoa wito kwa Shirika la Bandari kuziimarisha Bandari zake zote ikiwemo kuharakisha ujenzi wa bandari ya mpya Mangapwani ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto za kibandari ziliopo hivi sasa.

Kamati pia, inaishauri Wizara kupitia Shirika la Meli kuangaliwa kwa jicho la pekee suala zima la kupatiwa mafunzo maafisa wa meli ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuendana na mabadiliko ya utumiaji wa vyombo vya kisasa.

***Mheshimiwa Spika,*** Pia, kamati inalitaka shirika kufatilia na kuchukua hatua zinazofaa kuhakikisha wanaweka sawa mfumo mzuri kwa mishahara na maslahi ya mabaharia ambao utatambulika katika taasisi za kiutumishi Serikalini.Kamati inahimiza kutekelezwa maagizo yaliyotolewa na Serikali kuhusiana na kuuzwa kwa meli zake zisizofanya kazi ili kupunguza hasara inayopatikana kwa kuendelea kuwepo kwake.

Vile vile kamati inaitaka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, kupitia Wizara ya Uchukuzi, Miundombinu na Mawasiliano kuhakikisha wanaweka uzio na kupatikana hatimiliki kwa viwanja vya ndege Unguja na Pemba ili kuzuia kuvamiwa na wananchi.

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kamati inasikitishwa na hali inayoendelea hivi sasa ya msongamano wakati wa uchukuaji mizigo kwa abiria wa ndani na nje ya nchi kwa kiwanja chetu cha ndege cha Abeid Amani Karume kuwa na sehemu moja ya kupokelea mizigo kunakopelekea vurugu na kusubiria mizigo kwa muda mrefu. Hivyo basi, kamati inashauri kuchukuliwa hatua za makusudi kutenganisha mizigo ya safari za ndani na nje ya nchi ili kuondokana na usumbufu uliopo sasa ikiwemo mrundikano wa abiria wanaousubiri mizigo na hali halisi ya magonjwa ya uviko 19.

***Technolojia ya Habari na Mawasiliano***

***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti yetu pia inafafanua kwa upana wake Sekta ya Technolojia ya Habari na Mawasiliano inayotekelezwa na Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA pamoja na Idara ya Mawasiliano. Sekta hii kama zilivyo sekta nyingi zilizochini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi nayo inakubwa na matatizo mengi ikiwemo Kuwepo na uharibifu wa miundombinu ya Mkongo wa Taifa.

Kamati inashauri kutolewa zaidi elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa Mkongo wa Taifa na kuchukuliwa hatua kwa atakaebainika kuhujumu miundombinu ya Mkongo wa Taifa. kutoa matumizi sahihi ya utumiaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa wananchi Idara imeendelea kuratibu huduma za mawasiliano ya simu, internet na Posta Zanzibar.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaihimiza Wizara kuendelea kutoa matumizi sahihi ya utumiaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa wananchi Idara imeendelea kuratibu huduma za mawasiliano ya simu, internet na Posta Zanzibar.

***Ofisi Kuu Pemba***

***Mheshimiwa Spika,*** licha ya Ofisi Kuu Pemba kuendelea kujikongoja na kujitahidi kufanya shughuli zake bado inakabiliwa na mapungufu mbai mbali ikiwemo Uchakavu wa jengo, Mrundikano wa madeni ya fidia za nyumba pamoja na vipando kwa barabara zilizojengwa muda mrefu pamoja na Upungufu wa upatikanaji fedha za kuendeshea kazi hali inayopelekea kutotekelezwa shughuli za ofisi kama ilivojipangia. Kamati yetu inaishauri na kuiagiza Wizara kusawazisha changamoto zoto zilizoibuliwa ndani ya Ripoti yetu.

***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti yetu inamalizia kuichambua Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa kuelezea ziara ya kikazi ya Kamati na taasisi za Wizara hii huko Tanzania Bara. Kamati ilitembelea Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) pamoja na Shirika la Posta Tanzania. Kamati inatoa wito kwa Wizara kushirikiana na Shirika la Posta pamoja na TTCL kuendelea kutolewa elimu na kujenga uelewa kwa Wananchi wa Zanzibar ili waweze kuitumia taasisi hizo.

**WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI**

***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti yetu pia imechambua muundo na utendaji wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ambayo inadhamana ya ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata makaazi bora, salama na nafuu kupitia Programu yake ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi pamoja na Programu ya Usimamizi wa Ardhi na Makaazi.

***Sekta ya Uendeshaji***

***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti yetu inabainisha kasoro kubwa inayoikabali Sekta ya uendeshaji Katika Wizara hii ambayo ni Upungufu wa wafanyakazi wenye fani za kitaalamu, Uchelewaji wa upatikanaji wa vibali vya ujenzi pamoja na Ukosefu wa hatimiliki kwa nyumba zinazomilikiwa na wizara. Kamati inashauri kuchukuliwa hatua za haraka katika kutafuta wafanyakazi wataalamu, vibali vy ujenzi pamoja na hatimiliki kwa majengo ya Serikali ili kuondosha changamoto zinazoweza kujitokeza.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ilipofuatilia uendeshaji wa Wizara kwa upande wa Pemba imebaini Ufinyu wa bajeti na upungufu mkubwa wa wafanyakazi wataalamu katika sekta zote za Wizara hii. Aidha Kamati imekuta Upungufu wa vitendea kazi, pamoja na Uchakavu wa baadhi ya nyumba za Serikali. Ni Matumani ya Kamati kwamba, wizara itaongeza bajeti kwa Ofisi kuu Pemba ili iweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi pamoja na kununua vitendea kazi kama vile vifaa vya kupimia na magari.

***Mheshimiwa Spika,*** pia Kamati inashauri kutengwe fedha maalum kwa ajili ya matenngenezo ya nyumba Serikali katika bajeti ijayo. Kamati pia inapendekeza kufanyiwa haraka suala la wafanyakazi wataalamu ili waweze kusaidia kuleta ufanisi katika kukamilisha majukumu ya wizara Pemba.

***Usimamizi wa Ardhi na Makaazi***

***Mheshimiwa Spika,*** masuala ya Usimamizi wa Ardhi na Makaazi nayo tumeyazungumza kwa kina katika Ripoti yetu. Ripoti imefafanua tatizo la ufinyu wa Bajeti, na uhaba wa vitendea kazi unayoikabili Mahakama ya Ardhi pamoja na migogoro ya ardhi isiyokua ya lazima. Kamati inaendelea kushauri jengo linalomilikiwa na ZECO liliopo pembezoni mwa Mahkama ya Ardhi Mwanakwerekwe kupatiwa Mahkam ya Ardhi ili waweze kupunguza changamoto walonayo ya ufinyu wa ofisi hali ambayo inakwaza katika utendaji kazi. Vile vile Kamati inashauri kuangaliwa kwa jicho la huruma Mahkama hii na kupatiwa usafiri ambao umekua ni changamoto kubwa kwao kwa Unguja na Pemba.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha kuwepo na mashirikiano yakutosha kutoka katika taasisi zote ambazo kwa namna moja au nyengine zinahusika na masuala ya ardhi ili kuweza kuzuia na kupunguza migogoro ya ardhi ambayo kila siku imekua ni kilio katika nchi yetu na kusababisha athari mbalimbali kwa jamii. Pia Kamati inaitaka Mahkama kuzidi kufanya kazi kwa uweledi na sheria za nchi.

***Mheshimiwa Spika,*** usalama wa umiliki wa ardhi na upimaji wa ardhi, utambuzi na usajili wa ardhi, mipango ya miji na matumizi ya ardhi, ukarabati wa nyumba za maendeleo na majengo ya Serikali ni miongoni mwa Shughuli za Wizara hii. Shughuli hizi zinatekelezwa kupitia Kamisheni ya Ardhi, Mthamini Mkuu wa Serikali, Wakala wa Majengo, Shirika la Nyumba Zanzibar, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba, Bodi ya Kondomino, Bodi ya Usajili, Wasanifu Wahandisi na Wakadiriaji wa Majengo.

***Mheshimiwa Spika,*** Sekta hii nayo inakabiliwa na kasoro kadhaa kama zilivyoainishwa kwa kina katika ripoti yetu, Kamati inashauri Wizara kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya masuala yote ya Ardhi ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima katika jamii. Vile vile Kamati inasisitiza kuchukuliwa

hatua za haraka suala la uvamizi wa ardhi za Serikali, kilimo na eka 3 ili kuepusha athari za kimazingira pamoja na upotevu wa ardhi kiholela usiozingatia sheria na taratibu zilizowekwa.

## WIZARA YA MAJI NISHATI NA MADINI

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya tatu inayosimamiwa na Kamati yetu ni Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Wizara ambayo inadhamana ya kutoa huduma bora za maji, nishati na madini kupitia Programu ya Usimamizi wa Huduma za Maji, Programu ya Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini pamoja na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya Wizara.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati yetu pamoja na kuthamini juhudi na mipango mizuri na mikubwa ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa kila mwananchi, lakini inasikitishwa na changamoto kadhaa zinazokwaza utekelezaji wa Programu hii.

### *Sekta ya Maji*

Pamoja na taarifa mbali mbali za utekelezaji wa ZAWA na Idara ya, taasisi ambazo ndizo watekelezaji wakuu wa Programu hii, Kamati ilikaguwa vijiji mbali mbali vya Unguja na Pemba ambapo kwa ujumla Kamati imebaini changamoto kadhaa za ZAWA pamoja na Sekta ya maji kwa ujumla.

***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti yetu imebainisha kwa kina Changamoto za utekelezaji zinazokwaza sekta ya Maji ikiwemo tatizo la uzalishaji na uvuna wa maji, tatizo jengine ni uhababa wa Miundombinu na Uhifadhi wa Maji, huku hali ya  mivunjo na kuchakaa kwa mabomba nayo ikichangia kwa kiasi kikubwa changamoto za Sekta ya Maji. Kamati pia inaendelea kusononeshwa na hali ya madeni hasa kwa taasisi za serikali pamoja na ufinyu wa Bajeti inayoviza utekelezaji wa ZAWA na Idara ya Maji kwa ujumla.

Vile vile kwa masikitiko makubwa, Kamati inashangazwa na hali ya fedheha kutokana na uvamizi wa maeneo ya Vianzio vya Maji pamoja na Vitendo vya Hujuma za Miundombinu ya maji licha ya kwamba mengi ya maeneo hayo yanalindwa muda wote. Kamati inashauri wahalifu hao watafutwe na wachukuliwe hatua zinazostahiki dhidi yao.

***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na Changamoto tulizozibaini, Kamati inaishauri Wizara kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar kuwa na mpango wa kutumia Maji ya ZAWA kwa matumizi ya kawaida tu na ya kijamii, na sio shughuli nyengine za biashara na uzalishaji kama vile Matofali, kilimo, ukoshaji wa vyombo vya moto, na mengineyo. Kamati pia inaishauri ZAWA kuingia katika mifumo ya kisasa ili iweze kugundua hitilafi katika vianzio na miundombinu yake ya maji badala ya kusubiri kupewa taarifa na wananchi.

***Sekta ya Umeme***

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati pia kwa mara kadhaa ilipokea taarifa za utekelezaji wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO). **Kamati inasisitiza haja ya kuwepo kwa mashirikiano ya karibu ya kiutendaji miongoni mwa Watendaji wa Shirika hilo ili kuongeza kasi na ufanisi ulliokusudiwa. Kamati inaamini kwamba mashirikiano hayo ndio chachu ya mafanikio ya Shirika hilo na kupunguza malalamiko ndani ya watendaji wenyewe na pia kwa wateja wao.**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ilitembelea Kituo cha umeme cha Ras Kiromoni. Kamati yetu inawasiwasi wa mapato kwani imebaini kwamba, katika line namba 2 (Line Mpya) pia line hiyo imekuwa ikitumika kwa mawasiliano ya Kampuni ya Simu ya Zantel pamoja na Mkongo wa Taifa kupitia Fiber ya ZECO ndani ya Line hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti yetu pia imegusia azma ya TANESCO ya kutaka kuiuzia umeme ZECO kwa **shilingi 130.0 kwa Unit Moja** lakini bodi ya wakurugenzi ya ZECO bado haijakaa ili kujadili na kuidhinisha bei hiyo iliyopendekezwa. Hivyo Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha kuwa Bodi ya Wakurugenzi ya ZECO inakaa na kuridhia bei ya hiyo mpya ili baadae iwasilishwe EWURA kwa ajili ya kuidhinishwa na kuanza kutumika. Vile vile Kamati inaishauri Wizara kupitia Shirika la Umeme la

Zanzibar kuendelea kutoa elimu kwa wananchi wanaofanya shughuli zao za kijamii na wanaozunguka ndani ya maeneo ya miundombinu ya umeme.

***Udhibiti ya Huduma za Maji na Umeme***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu imeridhika na taarifa za ukaguzi wa ZURA katika miundombinu ya Maji na Umeme lakini kwa masikitiko kabisa inashangazwa na mrejesho wa taasisi hizo zilizokaguliwa kwa Mdhibiti. Miongoni mwa Changamoto zilizogunduliwa na ZURA na kuwasilishwa kwa Kamati ni kama zifuatazo: -

i. Kukosekana kwa uzio, vifaa vya usalama katika vituo vya maji (**pump house),** pamoja na mazingira machafu sana kwa baadhi ya vituo na baadhi ya visima kutokua na mifuniko sehemu ya juu (**Well Head).**

ii. Uwepo wa makaazi ya watu karibu na vyanzo vya maji.

iii. Kutofanya kazi kwa baadhi ya visima kutokana na kuungua kwa pump.

iv. Ufungaji ovyo wa Wanyama katika maeneo ya vyanzo vya maji.

**Mheshimiwa Spika,** hali kama hiyo ya kusikitisha pia imegunduliwa baada ya ZURA kufanya ukaguzi wa vituo vitano (5) vya kupozea umeme kwa ajili ya kulisha katika maeneo ya Mazizini, Jangombe, Bambi, Kilimahewa, Dole na Maruhubi pamoja na maeneo yote ya mjini. Kufuatia ukaguzi huo imebainika kuwa: -

i. Kituo cha Mwanyanya kipo karibu na jaa mita tano tu kutoka kituoni.

ii. Vituo vyote havina kisanduku cha huduma ya kwanza.

iii. Kituo cha Mpendae kinahitaji kuwekewa vipoza joto kama vile feni, Aircondition au feni za kutolea hewa nzito nje.

iv. Vituo vya Mpendae na Welezo tayari vimezidiwa ambapo hupelekea mpaka transfoma zake kuzima kipindi cha matumizi makubwa ya umeme.

***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyengine Kamati yangu imeshtushwa na kushangazwa na Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini iliyowasilishwa kwa Kamati kwa Kipindi cha Oktoba – Disemba, 2021. Kwa mujibu wa tarifa hiyo Muundo wa ZURA hauakisi utekelezaji wa majukumu ya Mdhibiti. Aidha kumekuweko na Mgongano wa majukumu baina ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini na Mamlaka (ZURA). Hivyo, kutokana na changamoto

hizo Kamati inaishauri Wizara ikae na ZURA na kutafuta mshauri elekezi wa kuweza kupamanua baina ya majukumu ya Wizara na Mamlaka.

***Bohari za Mafuta***

***Mheshimiwa Spika,*** kwa nyakati tofauti Kamati yetu ilitembelea Bohari za kuhifadhia mafuta za Wesha na Mtoni ambapo imeshuhudia kuwepo kwa njia za watembea kwa miguu pamoja na kuendelea kwa shughuli nyengine za kijamii kama vile kilimo, ufugaji na uvuvi katika maeneo yanayozunguka Bohari hizo suala ambalo Kamati inadhani sio sahihi kulingana na unyeti wa sehemu hizo.

***Mheshimiwa Spika,*** Bohari Kuu ya kuhifadhia mafuta ya Pemba huko Wesha inahitaji kuangaliwa kwa namna ya kipekee. Kamati ilishtushwa na hali iliyoikuta katika Bohari hiyo iliyojengwa miaka mingi iliyopita, kwani inakabiliwa na matatizo kadhaa ikiwemo Miundombini Chakavu, Tatizo la Usalama wa kiafya, kimazingira na kiulinzi, Eneo la kukusanyika wakati wa dharura (**Assembling Point**), Masafa baina ya tangi moja na jengine, Kupungua kwa kina cha maji pamoja na Uwezo mdogo wa matangi ya kuhifadhia mafuta.

***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na hali hiyo Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kujenga Matangi mapya kwa lengo la kukabiliana na changamoto iliyopo ya uchakavu wa Miundombinu ya kuhifadhi nishati ya mafuta kulingana na ongezeko la mahitaji ya nishati hiyo. Vile vile Kamati inazishauri taasisi zote zinazohusika na Bohari za Wesha na Mtoni kushirikana kwa pamoja na hatimae kulipatia ufumbuzi suala shughuli za kibinadamu katika maeneo yanayozinguka maeneo hayo ili kuepusha athari ambayo ikitokea itasababisha janga kubwa.

***Mheshimiwa Spika,*** kamati pia ilibaini katika ziara zake kuwepo na uhaba wa mashine za kupimia vinasaba vya mafuta kwa Unguja na Pemba. Hivyo, kamati imeona kuna haja ya kuongezwa mashine hizo ili kuweza kusaidia katika suala zima la kuangalia ubora wa mafuta yanayoingizwa nchini.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi inakamilisha Ripoti yake ya Mwaka 2021/2022 kwa kuwapongeza na kwa dhati Mawaziri, Makatibu Wakuu, pamoja Viongozi na watendaji wote kwa Ujumla wa Wizara zote tatu zinazosimamiwa na Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake ya Kikatiba na Kikanuni.

Aidha, Kamati inatoa shukurani za kipekee kwa Maafisa Wadhamini wa Wizara hizi pamoja na wasaidizi wao wote kwa mashirikiano mazuri waliyoipatia Kamati wakati wote Kamati ilipokuwa Kisiwani Pemba katika kutekeleza majukumu yake.

Vilevile, Kamati inatambua, kuthamini na Kushukuru ushirikiano ulipata kutoka kwa Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ suala mbalo lilipelekea kufanikisha shughuli zake zilizojipangia huko Tanzania Bara kwa ufanisi mkubwa.

Aidha kwa umuhimu mkubwa Kamati inakupongeza kwa dhati wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na sekretariati yote ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha vyema Kamati kutekeleza majukumu yake na kuweza kutayarisha ripoti yake kwa mwaka 2021/2022. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata ili kuweza kufikiwa malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho nawaomba waheshimiwa wajumbe kuisoma, kuichangia na hatimae kuikubali ripoti yetu ili hatimae kuongeza uwajibikaji na ufanisi bora na wenye tija katika nchi yetu. Ahsanteni sana kwa kuniskiliza.

**Mheshimiwa Spika** naomba kuwasilisha na naomba kutoa hoja.

**............................**

**(Mheshimiwa Yahya Rashid Abdulla),**

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati,**

**Baraza la Wawakilishi,**

**ZANZIBAR.**